# MAJI TANZANIA

TOLEO NA 020

APRILI- JUNI, 2023


# Dkt. JK aipongeza Wizara ya Maji Kufanikisha TanWIP

Wizara ya Maji imepongezwa kwa kukamilisha Programu ya Uwekezaji katika Sekta ya Maji (TanWIP) 2024-2030 hapa nchini, ambayo utekelezaji wake utakuwa na thamani ya Dola za Marekani Bilioni 15.02

Rais wa mstaafu wa Awamu ya Nne Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete ametoa pongezi hizo alipoongea na menejimenti ya taasisi za Sekta ya Maji jijini Dodoma, katika ukumbi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA).





# Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka 2023/2024

## Wizara ya Maji yatakiwa kutekeleza mwongozo wa ubia na sekta binafsi

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) ameitaka Wizara ya Maji ishirikiane na wadau mbalimbali wa sekta ya maji ili kutengeneza na kutekeleza mwongozo wa ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) ili kuimarisha uwekezaji katika Sekta ya Maji.



# Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka 2023/2024



Jumatano ya tarehe 10 Mei, 2023, Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Hamidu Aweso (Mb), aliwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka 2023/2024. Ufuatao ni muhtasari wa Bajeti hiyo ambayo imegawanyika katika maeneo makuu yafuatayo; Hali ya Sekta ya Maji Nchini; Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2022-2023; Mafanikio ya Miaka Miwili ya Serikali ya Awamu ya Sita katika Sekta ya Maji, Changamoto zilizojitokeza na hatua zilizochukuliwa; Vipaumbele na mpango wa utekelezaji kwa mwaka 2023/2024; na maombi ya fedha kwa mwaka 2023/2024.

**1. HALI YA SEKTA YA MAJI NCHINI**

1. Maelezo kuhusu hali ya Sekta ya Maji nchini kwa kuzingatia hali ya rasilimali za maji; ubora wa maji; na upatikanaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira vijijini na mijini.

2.1 Hali ya Rasilimali za Maji

2. Rasilimali za maji zilizopo nchini ni wastani wa mita za ujazo bilioni 126 kwa mwaka ambapo juu ya ardhi ni mita za ujazo bilioni 105 na ardhini ni mita za ujazo bilioni 21. Hivyo, kiasi cha maji kilichopo kwa kila mtu kwa mwaka ni wastani wa mita za ujazo 2,105. Hii ni kwa idadi ya watu milioni 59.8 waishio Tanzania Bara kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2022. Kiwango hicho ni juu ya wastani wa mita za ujazo 1,700 kwa mtu kwa mwaka kinachokubalika kimataifa. Hivyo nchi haijaingia kwenye uhaba wa mahitaji ya maji.

3. Takwimu zinaonesha kwamba nchi yetu inatarajiwa kufikia kiwango cha wastani wa mita za ujazo 1,700 kwa mwaka kwa mtu ifikapo mwaka 2030. Aidha, takwimu zinaonesha kwamba mahitaji ya maji nchini kwa sekta mbalimbali mwaka 2022 yalikuwa ni wastani wa mita za ujazo bilioni 62 na yanatarajiwa kufikia mita za ujazo bilioni 75 mwaka 2030. Hivyo, tunao wajibu wa kuendelea kuongeza msukumo katika utunzaji wa rasilimali za maji, kuongeza ufanisi katika matumizi ya maji pamoja na kuongeza upatikanaji wa maji ikiwa ni pamoja ujenzi wa mabwawa.

2.2 Hali ya Ubora wa Maji

4. Ubora wa maji ni kigezo muhimu katika kutoa maamuzi juu ya matumizi mbalimbali ya maji. Hali ya ubora wa maji katika maziwa, mito, mabwawa, chemichemi na visima inakidhi viwango hivyo vinaweza kuendelezwa na kutumika kwa matumizi mbalimbali ya shughuli za kiuchumi, kijamii na mazingira. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuwekeza katika teknolojia mbalimbali za kusafisha na kutibu maji ili kuhakikisha maji yanayotumika yanafaa kwa matumizi yaliyokusudiwa.

2.3 Hali ya Upatikanaji wa Huduma ya Maji Vijijini

5. Hali ya upatikanaji wa huduma za maji vijijini imeongezeka kutoka wastani wa asilimia 74.5 mwezi Desemba, 2021 hadi kufikia wastani wa asilimia 77 mwezi Desemba, 2022. Kiwango hicho kimeongeza idadi ya wananchi wanaopata huduma ya maji kwenye maeneo ya vijijini kufikia 30,209,409 hivi sasa

2.4 Hali ya Upatikanaji wa Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini

6. Hali ya huduma ya majisafi na salama katika maeneo ya mijini imeongezeka kutoka wastani wa asilimia 86.5 mwezi Desemba, 2021 hadi wastani wa asilimia 88 mwezi Desemba, 2022. Kiwango hicho kimeongeza idadi ya wananchi 2,345,537 wa maeneo ya mijini wanaopata huduma ya maji.

7. Huduma ya uondoshaji majitaka katika maeneo ya mijini imeendelea kuimarika ambapo mtandao wa mabomba ya majitaka umeongezeka kutoka kilomita 1,385.8 mwezi Aprili 2022 hadi kufikia kilomita 1,416.93 mwezi Aprili 2023. Aidha, kwenye miji ya Geita, Kahama, Magu, Misungwi, Lindi, Kigoma, Sumbawanga, Bukoba na Lamadi ambayo haina mtandao, huduma ya uondoshaji majitaka inatolewa kwa utaratibu wa magari na mabwawa ya kutibu majitaka.

**3.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2022/23**

3.1 Upatikanaji wa Fedha

8. Mwaka 2022/23, Fungu 49 – Wizara ya Maji iliidhinishiwa jumla ya Shilingi bilioni 709.36; kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 51.46 ni fedha za matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni 657.89 ni fedha za maendeleo. Hadi mwezi Aprili 2023, Wizara imepokea jumla ya Shilingi bilioni 686.37 sawa na asilimia 96.76 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa, Shilingi bilioni 648.08 ni za kutekeleza miradi ya maendeleo na Shilingi bilioni 38.29 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

3.2 Programu na Miradi Mbalimbali Iliyotekelezwa katika mwaka 2022/23

9. Wizara imeendelea kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi na mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo:-

3.2.1 Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

10. Usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji unahusisha tathmini na ufuatiliaji wa rasilimali za maji; kuhifadhi na kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji; kugawa maji kwa sekta mbalimbali kwa kuzingatia mahitaji na kiasi cha maji kilichopo; na kuendeleza rasilimali za maji. Hadi mwezi Aprili 2023, vituo 136 vya kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji vimekarabatiwa na vituo sita (6) vimejengwa; vibali vipya 1,554 vya matumizi ya maji na vibali 630 vya kuchimba visima vya maji vimetolewa; leseni 105 zimehuishwa; na

vyanzo 63 vimewekewa mipaka. Vilevile, ujenzi wa mabwawa 10 ya ukubwa wa kati na madogo umekamilika na ujenzi wa mabwawa 40 unaendelea.

11. Naomba niwahimize wananchi wote wanaotaka kutumia maji kutoka katika vyanzo mbalimbali wafahamu kuwa wanao wajibu wa kisheria wa kuomba vibali vya matumizi ya maji kutoka katika Bodi za Maji za Mabonde.

3.2.2 Huduma za Ubora wa Maji

12. Mwaka 2022/23, Wizara ya Maji kupitia Maabara za Ubora wa Maji imeendelea kusimamia na kufuatilia ubora wa maji nchini. Vilevile, Wizara imeendelea kuhakiki na kufuatilia ubora wa madawa ya kusafisha na kutibu maji pamoja na kuhakiki ubora wa majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira. Jumla ya vyanzo vya maji 1,473 ambavyo ni mito, maziwa, chemichemi na mabwawa vilihakikiwa ubora wake. Matokeo ya uchunguzi yalionesha kuwa ubora wa maji wa vyanzo vya maji nchini na mitandao ya kusambaza maji ni wa kuridhisha.

13. Natoa wito kwa wadau wote kutambua umuhimu wa kupima maji kabla ya kuyatumia kwa matumizi mbalimbali.

3.2.1 Huduma za Usambazaji Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini

14. Mwaka 2022/23, Serikali kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) ilipanga kutekeleza jumla ya miradi 1,029 ya maji na usafi wa mazingira vijijini. Hadi mwezi Aprili 2023, jumla ya miradi 586 imekamilika na miradi mingine utekelezaji wake unaendelea.

15. Katika kuhakikisha miradi ya maji vijijini inakuwa endelevu, hadi mwezi Aprili 2023, jumla ya vyombo 111 vya Watoa Huduma ngazi ya Jamii (CBWSOs) vimeundwa na kusajiliwa na hivyo kuwa na jumla ya CBWSO 2,515 zilizosajiliwa. CBWSOs hizo zimeajiri jumla ya wataalam 5,296 kwa ajili ya uendeshaji. Vilevile, Serikali imeendelea kuzijengea uwezo CBWSOs kwa kutoa mafunzo maalum kuhusu utunzaji, uendeshaji na usimamizi wa miradi ya maji vijijini; kununua vitendea kazi; na kujenga majengo ya ofisi.

16. Wizara ya Maji kupitia RUWASA inatekeleza Programu ya Uendelevu wa Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Program for Results-P4R) ambapo fedha hutolewa kutokana na matokeo ya utendaji. Awali, Programu hii ilianza kutekelezwa katika mikoa 17 (Geita, Iringa, Kagera, Katavi, Kigoma, Lindi, Manyara, Mara, Mtwara, Mwanza, Rukwa, Ruvuma, Shinyaga, Simiyu, Singida, Songwe na Tabora). Awali Programu hiyo ilitengewa Dola Milioni 350, katika kipindi cha miaka miwili ya utekelezaji wake, programu imeonesha mafanikio yaliyopelekea Benki ya Dunia kuongeza kiasi cha Dola za Marekani Milioni 300 na kufanya kuwa na jumla ya Dola Milioni 650.

17. Fedha zinazotolewa zinatokana na matokeo ya utendaji ambapo anayefanya vizuri anapata fedha nyingi zaidi. Kwa mfano Halmashauri ya Nzega ilianza kwa kupewa fedha za awali Shilingi Bilioni 1.3 mwaka 2020/21 na mwaka 2022/23 imeweza kupata Shilingi Bilioni 10.3. Kutokana na utendaji mzuri na kuongezeka kwa fedha, programu itatekelezwa katika mikoa 25. Mikoa iliyoongezeka ni Njombe, Mbeya, Morogoro, Pwani, Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Dodoma ambapo kwa kila Halmashauri ya Wilaya itapewa Shilingi Milioni 961 kama fedha za awali.

3.2.2 Huduma za Usambazaji wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini

18. Serikali kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutekeleza miradi ya majisafi na usafi wa mazingira katika miji mbalimbali. Katika mwaka 2022/23, jumla ya miradi 175 ilipangwa kutekelezwa ambapo hadi mwezi Aprili 2023, miradi 40 imekamilika na miradi 135 inaendelea kutekelezwa na ipo kwenye hatua mbalimbali. Baadhi ya miradi ni kama ifuatavyo:-

(a) Mradi wa Kuboresha Huduma ya Maji katika Jiji la Mbeya

19. Serikali imeanza utekelezaji wa mradi wa kutoa maji kutoka chanzo cha Mto Kiwira kupeleka katika Jiji la Mbeya kwa gharama ya Shilingi bilioni 117. Mradi huo utaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 66.5 hadi lita milioni 184 kwa siku na kuimarisha hali ya huduma ya maji kutoka asilimia 80 hadi asilimia 95.

(b) Mradi wa Kuboresha Huduma ya Maji katika Jiji la Dodoma

20. Katika mpango wa muda mfupi wa kuboresha huduma ya maji katika Jiji la Dodoma, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa maji Nzuguni unaogharimu Shilingi bilioni 5. Mradi huo utaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 68.7 hadi lita milioni 76.3 kwa siku na utawanufaisha wakazi wa maeneo ya Nzuguni, Ilazo, Swaswa na Kisasa.

21. Serikali inaendelea kutafuta vyanzo vya maji vya uhakika kwa ajili ya Jiji la Dodoma ikiwemo ujenzi wa Bwawa la Farkwa na kutoa maji Ziwa Victoria.

(c) Miradi ya Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Mkoa wa Dar es Salaam na baadhi ya Maeneo ya Mkoa wa Pwani

22. Serikali inatekeleza miradi ya kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na miji ya Kibaha, Kisarawe, Mkuranga, Chalinze na Bagamoyo katika Mkoa wa Pwani. Baadhi ya miradi hiyo ni pamoja na mradi wa ukarabati na upanuzi wa mfumo wa kusambaza majisafi ambao umekamilika na kuzinduliwa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 16 Machi, 2023; mradi wa usambazaji maji maeneo ya Mbezi – Makabe; na ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji kutoka katika visima virefu vya Kimbiji na Mpera. Katika kuhakikisha maji yanapatikana kwa kipindi chote cha mwaka, Serikali imeanza ujenzi wa bwawa la Kidunda na mkandarasi yupo eneo la kazi na malipo ya awali shilingi bilioni 49 yamefanyika.

(d) Mradi wa Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Jiji la Mwanza

23. Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya pamoja na Shirika la Maendeleo la Ufaransa imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa miundombinu ya kusafisha na kutibu maji katika eneo la Butimba kwa gharama ya Euro 26,165,102 (sawa na shilingi bilioni 69). Hadi mwezi Aprili 2023, utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 71. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2023 na utawanufaisha wakazi wa maeneo ya Jiji la Mwanza (Nyegezi, Mkolani, Buhongwa, Nyamazobe, Nyahingi, Bugando, Luchelele, Lwanima, Sahwa, Fumagila, Kishiri na Igoma); Magu (Kisesa, Bujola na Kanyama) na Wilaya ya Misungwi (Usagala, Fela, Bukumbi na Nyashishi).

(e) Mradi wa Maji Mugango – Kiabakari - Butiama

24. Serikali inatekeleza mradi wa maji Mugango - Kiabakari - Butiama kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 30.69 (sawa na shilingi bilioni 70.5). Hadi mwezi Aprili 2023, utekelezaji wa mradi ulikuwa umefikia asilimia 79 na unatarajiwa kukamilika katika mwaka 2023/24. Mradi huo utawanufaisha wakazi 100,000 waliopo katika eneo la mradi pamoja na vijiji vilivyopo ndani ya kilomita 12 kutoka bomba kuu.

(f) Simiyu Mradi wa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika Mkoa wa Simiyu

25. Mradi wa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi unatekelezwa kwenye Wilaya tano (5) za Busega, Bariadi, Itilima, Maswa na Meatu katika Mkoa wa Simiyu. Mradi huo unatekelezwa na Serikali kwa gharama ya Shilingi bilioni 444.6. Hadi mwezi Aprili 2023, kiasi cha Shilingi bilioni 1.97 kimetumika kulipa fidia kwa wananchi wapatao 1,364 kati ya 1,395 waliofanyiwa uthamini. Aidha, taratibu za kuwapata wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa mradi zinaendelea na utekelezaji unatarajiwa kuanza katika mwaka 2023/24.

(g) Mradi wa Kuboresha Huduma ya Maji katika Miji 28

26. Serikali imeanza utekelezaji wa mradi wa uboreshaji huduma ya maji katika miji 28 unaogharimu Shilingi trilioni 1.48. Wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa mradi wamepatikana na wameanza maandalizi ya awali ya maeneo ya ujenzi pamoja na kukamilisha kazi ya usanifu. Miji itakayonufaika na mradi huu ni Kilwa Masoko, Nanyumbu, Makonde, Njombe, Makambako/Wangingómbe, Ifakara, Chunya, Rujewa, Singida, Kiomboi, Manyoni, Chamwino, Chemba, Mugumu, Tarime/Rorya, Sikonge, Urambo/Kaliua, Kasulu, Mpanda, Songea, Geita, Chato, Kayanga, Mafinga, Handeni, Korogwe, Muheza na Pangani.

(h) Miradi ya Maji katika Miji mingine

27. Miradi mingine inayoendelea kutekelezwa katika baadhi ya miji ni pamoja na; Majiji ya Arusha na Tanga; Manispaa za Morogoro, Shinyanga na Mtwara/Mikindani; na Mji wa Tunduma, Tinde na Shelui.

**4.0 MAFANIKIO YA MIAKA MIWILI YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KATIKA SEKTA YA MAJI**

28. Katika kipindi cha miaka miwili (2021 - 2022) ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wetu Mpendwa, mpenda wananchi wake, mwenye dhamira njema ya kumtua mama ndoo kichwani, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mafanikio makubwa yamepatikana katika Sekta ya Maji. Mafanikio hayo ni pamoja na:-
(i) Mageuzi makubwa ya kiutendaji yaliyofanyika kwa watumishi 9,422 waliopo ambao wamechangia mafanikio makubwa ya sekta kutokana na kuwa na ari ya kazi, kujituma, weledi na kubeba maono mema ya Rais wetu ya kumtua mama ndoo kichwani.
(ii) Kukamilika kwa miradi 1,373 ya usambazaji maji inayotoa huduma katika vijiji 2,649 na kufikisha jumla ya vijiji 9,737 vinavyopata huduma ya maji nchini;
(iii) Kukamilika kwa miradi 80 ya usambazaji maji mijini ambayo inatoa huduma kwa wananchi 4,305,801;
(iv) Kukwamuliwa kwa miradi 157 kati ya 177 ya maji vijijini iliyokuwa na changamoto kwa muda mrefu;
(v) Kuanzishwa kwa mfumo wa takwimu za miradi (MajiApp) na mfumo wa usimamizi wa ankara za maji (Unified billing system);
(vi) Kuongezeka kwa maabara za ubora wa maji zenye hadhi ya Ithibati kutoka maabara moja (1) ya Mwanza iliyokuwepo mwaka 2021 hadi kufikia maabara saba (7). Maabara hizo ni Singida, Shinyanga, Kigoma, Bukoba, Musoma na Dar es Salaam;
(vii) Kuanza kwa ujenzi wa mabwawa ya Kidunda na Farkwa;
(viii) Kununuliwa na kuanza kutumika kwa seti 25 za mitambo ya kuchimba visima na seti tano (5) za mitambo ya ujenzi wa mabwawa;
(ix) Kuzinduliwa kwa Mpango wa Uhifadhi wa Vidakio vya Maji nchini wa mwaka 2021 hadi 2035. Kupitia Mpango huo, jumla ya miti rafiki ya maji 2,541,803 imepandwa kwenye maeneo ya vyanzo vya maji katika mabonde yote tisa nchini; na
(x) Kufanyika kwa Marekebisho Na. 8 ya Mwaka 2022 ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009 ili kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini.

29. Katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama imeimarika kwa wananchi wa vijijini kutoka wastani wa asilimia 70.1 mwaka 2020 hadi asilimia 77 mwezi Desemba, 2022; na kwa maeneo ya mijini kutoka wastani wa asilimia 84 mwaka 2020 hadi wastani wa asilimia 88 mwezi Desemba, 2022.

**5.0 CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA NA HATUA ZINAZOCHUKULIWA**

30. Changamoto kubwa zinazoikabili sekta ya maji ni:-
a) Mahitaji makubwa ya fedha za uwekezaji kwenye miradi mikubwa ya maji hasa ya kimkakati;
b) Uharibifu wa vyanzo vya maji unaotokana na uvamizi na uchafuzi; na
c) Mabadiliko ya tabianchi.
31. Katika kukabiliana na changamoto hizo, hatua mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa zikiwemo kuendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mikubwa ya maji; kushirikiana na wadau katika kuendeleza uhifadhi na udhibiti wa uchafuzi wa vyanzo vya maji; kutekeleza miradi ya maji ambayo itatumia vyanzo vya maji vya uhakika kama vile mito mikubwa na maziwa; ujenzi wa mabwawa ya kuhifadhi maji; na kutekeleza mkakati wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

**6.0 VIPAUMBELE NA MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2023/24**

32. Mwaka 2023/24, Serikali imepanga kuwa na vipaumbele vifuatavyo:-
a) Kukamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002;
b) Kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji;
c) Kuwa na mtandao wa taifa wa maji (National Water Grid);
d) Kuwa na Mpango Kabambe wa Usambazaji Maji (Water Supply Masterplan);
e) Kuimarisha usimamizi wa ubora wa maji;
f) Kukamilisha ujenzi, ukarabati na upanuzi wa miradi inayoendelea na kukabiliana na upotevu wa maji (Non Revenue Water - NRW);
g) Kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ili kuwa na huduma endelevu ya upatikanaji wa maji;
h) Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa maji wa miji 28;
i) Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya usafi wa mazingira;
j) Kuendelea na ujenzi wa mabwawa madogo, yenye ukubwa wa kati na makubwa yakiwemo Kidunda na Farkwa ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;
k) Kuimarisha taasisi za Wizara ya Maji ikiwemo Chuo cha Maji, Mfuko wa Taifa wa Maji na RUWASA; na
l) Kuimarisha ushirikiano na ushirikishwaji wa wadau wa sekta ya maji.

**7.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2023/2024**

33. Ninaomba sasa kutoa hoja Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 756,205,106,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2023/24. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni Shilingi 60,375,474,000 ambapo Shilingi 18,035,561,000 ni kwa ajili ya kugharamia Matumizi Mengineyo (OC) na Shilingi 42,339,913,000 ni kwa ajili ya kulipa mishahara (PE). Jumla ya bajeti ya maendeleo ni Shilingi 695,829,632,000 ambapo kati ya fedha hizo, Shilingi 407,064,860,000 ni fedha za ndani na Shilingi 288,764,772,000 ni fedha za nje.
Bajeti inapatikana katika Tovuti ya Wizara ya Maji, yenye kikoa cha www.maji.go.tz

***PICHA: Matukio mbalimbali wakati Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akiwasilisha hotuba ya bajeti, Bungeni jijini Dodoma.***





# Wizara ya Maji yatakiwa kutekeleza mwongozo wa ubia na sekta binafsi






Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) ameitaka Wizara ya Maji ishirikiane na wadau mbalimbali wa sekta ya maji ili kutengeneza na kutekeleza mwongozo wa ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) ili kuimarisha uwekezaji katika Sekta ya Maji.

Amesema hayo wakati akizindua Mkakati Mpya wa Asasi ya WaterAid Tanzania 2023-2028 na Maadhimisho ya Miaka 40 ya Asasi hiyo nchini Tanzania jijini Dar es Salaam.

Waziri Mkuu amesema yapo mafanikio mengi yaliyoletwa na Wizara ya Maji lakini bado inatakiwa kuendeleza ushirikiano ili kuhakikisha fedha zinazotolewa zinafikisha huduma endelevu, jumuishi na salama ya majisafi, usafi wa mazingira na usafi binafsi kwa Watanzania wote.

Aidha, Wizara ya Maji kwa kushirikiana na wadau wa Sekta ya Maji ihakikishe miradi yote inayoendelea katika Sekta ya Maji inatekelezwa kwa ufanisi na inakamilika kwa wakati na kwa kuzingatia thamani ya fedha. Amesema hiyo itasaidia kufanikisha na kuharakisha uwekezaji katika Sekta ya Maji katika maeneo mbalimbali nchini.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) akimwakilisha Waziri wa Maji amewashukuru Asasi ya WaterAid Tanzania kwa kuwa tayari kusaidia Sekta ya Maji nchini. Amesema utekelezaji wa Mpango uliopita umewezesha ujenzi wa idadi ya miradi 73 inayojumisha miradi 14 ya maji, miradi 57 ya miundombinu ya WASH kwenye shule na vituo vya kutolea huduma za afya, na miradi 2 ya miundombinu ya udhibiti majitaka.




Utelekelezaji wa miradi hiyo umepelekea wananchi kupata majisafi na salama, vituo vya afya 35 kupata huduma ya maji na shule 30 zimepata miundombinu ya WASH ikiwemo miundombinu ya uvunaji maji ya mvua.

Awali akitoa salam za ukaribisho Mkurugenzi Mkazi wa Asasi ya WaterAid Tanzania. Anna Tenga Mzinga ameshukuru ushirikiano mzuri ambao wameupata kwa muda wote tangu waanze kazi nchini Tanzania. Amesema kwa miaka 40 iliyopita Asasi hiyo imewafikia watu milioni 8 moja kwa moja kwa huduma ya maji safi, kuwapatia watu 800,000 vyoo bora, na kuwafikia watu milioni 26 kwa uhamasishaji wa usafi wa mazingira wanaofanya kazi katika Mikoa 11 ya Tanzania Bara na Zanzibar.

# Dkt. JK aipongeza Wizara ya Maji Kufanikisha TanWIP



Wizara ya Maji imepongezwa kwa kukamilisha Programu ya Uwekezaji katika Sekta ya Maji (TanWIP) 2024-2030 hapa nchini, ambayo utekelezaji wake utakuwa na thamani ya Dola za Marekani Bilioni 15.02

Rais wa mstaafu wa Awamu ya Nne Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete ametoa pongezi hizo alipoongea na menejimenti ya taasisi za Sekta ya Maji jijini Dodoma, katika ukumbi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA).

Mhe. Dkt. Kikwete amesema hatua iliyopigwa na Serikali ya Awamu ya Sita ni kubwa kwa sababu lengo la "kumtua mama ndoo ya maji kichwani" linakamilishwa ikiwamo kuhakikisha maji yanapatikana ndani ya mita 400 kutoka katika makazi, na sio wananchi kusafiri kwenda kutafuta huduma ya maji.

Ameongeza kuwa mapinduzi na mabadiliko makubwa yamefanyika katika kuihudumia jamii katika eneo la maji, ukilinganisha na historia ilivyokuwa zamani pamoja na juhudi za dhati zilizokuwa zikifanywa na viongozi wa ngazi tofauti tofauti katika kufanikisha utekelezaji wa miradi wa maji.

Mhe. Rais Dkt. Kikwete katika historia ya uongozi wake aliteuliwa kuwa Waziri wa 10 kuhudumu katika Sekta ya Maji tangu nchi ilipopata uhuru mwaka 1961.

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akiongea katika kikao hicho amesema Sekta ya Maji na kazi zake kwa ujumla imebebwa na watu wengi, na viongozi mbalimbali akiwemo Mhe. Kikwete, ambaye alifanya kazi kubwa ya kutukuka na hadi leo bado anatumika kujenga kizazi kipya katika kazi.

Mhe. Aweso amesisitiza wazee katika jamii wana mchango mkubwa katika maendeleo yanayotokea leo na mabadiliko mbalimbali katika utendaji kazi, hivyo ni vizuri watumike.

Akielezea program hiyo ya TanWIP Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Mhandisi Nadhifa Kemikimba amesema imejikita katika maeneo makuu manne ambayo ni maji kwa uchumi endelevu, maji kwa ustawi wa jamii, masuala ya mabadiliko ya tabia nchi na menejimenti ya rasilimali za maji.

Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete ni Mwenyekiti wa Bodi ya Taaisi inayojishughulisha na masuala ya maji, Global Water Partnership Southern Africa (GWPSA) na Mwenyekiti Mwenza Mbadala (Alternative Co-Chair) wa Programu ya Uwekezaji katika Maji barani Afrika, Continental Africa Water Investment Programme (AIP) High-Level Panel.



# MORUWASA yapewa heko kwa kazi nzuri

Naibu Waziri wa Maji, Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) ameipongeza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) kwa kazi nzuri ya kutekeleza ujenzi wa mradi wa maji wa Magadu.

Naibu Waziri Mahundi ametoa pongezi hizo wakati wa ziara ya kikazi mkoani Morogoro ambapo amekagua mradi wa maji wa Magadu utakaonufaisha wananchi zaidi ya 23,000 wa maeneo ya kata hiyo kwa ufadhili wa serikali wa Tsh.Bilioni 1.7 kupitia Mfuko wa Taifa wa Maji.

Mhe. Mahundi amewasisitiza wananchi kuhakikisha wanatunza miundombinu na chanzo cha maji ili mradi huo kuwa endelevu kwa sasa na vizazi vijavyo.

Katika ziara hiyo, Mkuu wa Wilaya Morogoro Mhe. Rebeca Nsemwa ametoa pongezi kwa Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na watendaji wake wa Wizara ya Maji kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Na Mbunge wa jimbo la Morogoro Mjini Mhe. Dkt. Abdulaziz Abood (Mb) pamoja na Diwani wa Kata ya Magadu wameipongeza Wizara ya Maji kwa kazi nzuri na watendaji wa MORUWASA kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kutatua changamoto ya maji katika Manispaa ya Morogoro.

Mkurugenzi Mtendaji wa MORUWASA Mhandisi Tamim Katakweba amesema mradi huo upo katika hatua za mwisho na kutarajiwa kuanza kuhudumia wananchi kuanzia Julai 2023 na ameshukuru kwa fedha zilizotolewa na Serikali kufanikisha upatikanaji wa maji Morogoro kwa zaidi ya asilimia 100.

Katika ziara yake, Mhe.Mahundi pia ametembelea mradi wa kuhifadhi chanzo cha Maji mto Tangeni unaotekelezwa na Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu na kupongeza juhudi za utunzaji na uhifadhi wa vyanzo vya maji.

Naibu Waziri Mahundi amepongeza na kufurahishwa na ushirikiano uliopo baina ya Taasisi za Sekta ya Maji mkoani Morogoro.



Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Morogoro.



# MORUWASA watakiwa kuongeza kasi kukamilisha mradi wa bilioni 185





Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Mhandisi Nadhifa Kemikimba ameitaka Menejimenti ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) kuhakikisha inaongeza kasi katika utekelezaji wa mradi wa maji mkubwa wa Uboreshaji Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Manispaa ya Morogoro.

Amesema hayo akiwa katika ziara ya kikazi kwa taasisi za Sekta ya Maji mkoani Morogoro, na miongoni mwa aliokutana nao katika kikao kazi ni menejimenti ya MORUWASA kwa kufanya tathmini ya maendeleo ya utekelezaji wa mradi huo unaofadhiliwa na Serikali kupitia mkopo wenye masharti nafuu kutoka Shirika la Maendeleo la Ufaransa ( AFD) kwa thamani ya shilingi bilioni 185.

Mhandisi Kemikimba ameielekeza menejimenti ya MORUWASA na timu inayotekeleza mradi huo kufanya marejeo ya muda wa utekelezaji wa vipengele vya mradi ikiwemo unyanyuaji wa Bwawa la maji la Mindu, ujenzi wa mtambo mpya wa kutibu maji wa Mafiga wenye uwezo wa kuzalisha maji lita 54,000,000 kwa siku na ujenzi wa ofisi mpya za MORUWASA ili kuongeza kasi ya utekelezaji na kuhakikisha mradi unakamilika mapema na kwa wakati.

Katika ziara hiyo Katibu Mkuu Mhandisi Kemikimba ameongea na watumishi wa MORUWASA na kuwapongeza kwa kazi kubwa na jitihada wanazozifanya katika kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maji pamoja na kuendelea kutoa huduma ya maji kwa wananchi.

Aidha, amewasisitiza watumishi wa MORUWASA pamoja na jitihada kubwa wanazozifanya, bado wana kazi kubwa ya kufanya katika miradi ya maji na kuwataka kuendelea kufanya kazi kwa dhati.

# MWAUWASA watakiwa kutendea haki nafasi zao

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Cyprian Luhemeja amewataka watumishi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) kuhakikisha wanatumikia vyema nafasi zao ili kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi katika maeneo mbalimbali wanayohudumia.

Amesema hayo kwa nyakati tofauti wakati akitembelea ofisi mbalimbali za MWAUWASA ili kuzungumza na watumishi na kujadili changamoto zinazowakabili katika ufikishaji wa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi lengo likiwa ni kuzipatia ufumbuzi wa pamoja na kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji jijini Mwanza.

"Ninaamini MWAUWASA mnao uwezo wa kufanya vizuri zaidi katika kuwahudumia wananchi, nina imani mkijipanga vyema hali ya huduma ya maji itaimarika," Mhandisi Luhemeja alisema na kuongeza kuwa Jiji la Mwanza ni Jiji la kimkakati na kwamba linahitaji kuwa na huduma bora na ya uhakika ya majisafi na salama hasa ikizingatiwa kuwa Serikali imewekeza fedha nyingi kuhakikisha huduma inaimarika.

"MWAUWASA ni Mamlaka ya Maji ya pili kwa ukubwa baada ya DAWASA, mpo kimkakati na mkoa wa Mwanza ndio kitovu cha kanda ya ziwa na huu mkoa unaakisi masuala yote ya kiuongozi Kanda ya Ziwa," Mhandisi Luhemeja alisisitiza.

Aliwaasa watumishi wa MWAUWASA kuhakikisha wanatanguliza mbele uzalendo, nidhamu, ubunifu, kuheshimiana na kufanya kazi kwa pamoja kwa maslahi mapana ya wananchi wanaowahudumia.

Alisema Serikali imewaamini watendaji wa MWAUWASA na hivyo kuwapa dhamana ya kuwafikishia wananchi wa Mwanza huduma ya maji na aliwasisitiza kuhakikisha wanaienzi amana hiyo ili dhamira ya Serikali ifikiwe kikamilifu.

"Malalamiko ni mengi, hakikisheni mnajipanga vyema, mnasimamia kikamilifu usambazaji wa maji ili kufikisha huduma kote mnapopaswa kufikisha. Uzuri wa maji unaweza kuyahifadhi" Mhandisi Luhemeja alisema na kuainisha kuwa upotevu wa maji ni mkubwa na aliielekeza MWAUWASA kuhakikisha inajipanga na inakuja na mikakati dhabiti katika harakati za kupunguza upotevu wa maji ili kuongeza upatikanaji wa maji wanayozalisha.



*Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Mhandisi Cyprian Luhemeja akiwa na watumishi wa MWAUWASA wakati wa ziara yake ya kikazi Jijini Mwanza.*



# Ushrikishwaj wa wadau Sekta ya Maji wawaleta UKEF wa Uingereza



Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amefanya mazungumzo na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la UK Export Finance (UKEF), Bwn. Tim Reid kuhusu Sekta ya Maji na maendeleo yake hapa nchini.

Mazungumzo hayo yamefanyika jijini Dodoma ambapo ni matokeo ya ziara ya Mhe. Aweso aliyoifanya hivi karibuni nchini Uingereza na kufanya mazungumzo na wadau mbalimbali wa maendeleo kwa lengo la kushirikiana katika utatuzi wa changamoto zinazoikumba Sekta ya Maji nchini Tanzania.

Waziri Aweso katika mazungumzo hayo amemhakikishia Bwn. Reid kuwa serikali ya Tanzania iko tayari kushirikiana na UKEF katika kuhakikisha malengo yake yanafikiwa.

Amesema Wizara ya Maji ipo katika mipango mbalimbali mahsusi yenye lengo la kuhakikiha mama wa Tanzania anatua ndoo ya maji kichwani na jitihada hizo haziwezi kufanikiwa bila ushirikishwaji na kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo wakiwemo UKEF.

Kwa upande wake Bwn, Reid amemhakikishia Waziri Aweso kuwa UKEF iko tayari kushirikiana na Serikali ya Tanzania kutokana na utayari ambao ameuoneshwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na timu yake wakiwamo viongozi wa Wizara ya Maji katika kujenga ushirikiano na mataifa ya nje ikiwamo nchi ya Uingereza.

Amemuomba Waziri Aweso afikishe salam zake kwa Mhe. Rais kuwa UKEF wana imani kubwa na serikali anayoiongoza hivyo wako tayari wakati wowote kuendeleza ushirikiano huo kwa kupitia Sekta ya Maji.

Pamoja na Mhe. Aweso, katika kikao kimehudhuriwa na Katibu Mkuu Wizara ya Maji Mhandisi Nadhifa Kemikimba pamoja na wataalam wa Wizara ya Maji.

# Bilioni 12.6 kutunza maji ya Victoria Mwanza

Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria kupitia programu ya Pamoja ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji katika Bonde la Ziwa Victoria (LVB-IWRM) inatarajia kutumia kiasi cha Euro milioni 5.3, sawa na zaidi ya shilingi za Tanzania bilioni 12.6 ili kutekeleza ujenzi wa miundombinu ya majitaka na usafi wa mazingira jijini Mwanza.


Mradi huo utatekelezwa kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jiji la Mwanza (MWAUWASA) na utahusisha ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikiwemo mitaro yenye urefu wa takribani kilometa 15, ununuzi wa magari ya majitaka na kuunganisha kaya mbalimbali katika mfumo wa majitaka ili kuthibiti tabia ya kutapisha majitaka kutoka katika makazi kuelekea katika ziwa Victoria.

Naibu Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Bonde hilo Mhandisi Coletha Ruhamya ameainisha hayo wakati wa mafunzo maalumu kwa wanahabari jijini Mwanza yakiwahusisha na Maafisa Habari kutoka Wizara Mtambuka ikiwemo Wizara ya Maji.

Amesema programu hiyo ni kubwa na inahitaji ushirikishwaji wa makundi mbalimbali katika jamii ili kuhakikisha taarifa sahihi zinapatikana wakati wa utekelezaji.

Akifungua mafunzo hayo Mkurugenzi wa Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Viktoria Dkt. Renatus Shinhu amewashukuru wadau wa maendeleo katika mradi huo ambao ni European Union (EU), Serikali ya Ujerumani kupitia Benki ya KFW pamoja na Serikali ya Tanzania.

Amesema mradi huo utawezesha usalama wa Ziwa Victoria na kuokoa mimea na viumbehai wengine wanaotegemea maji ya ziwa hilo.
Programu ya Pamoja ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji ya Ziwa Victoria (LVB IWRMP) ni programu ya kikanda inayoratibiwa na Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria (LVBC) na kutekelezwa katika nchi tano wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.



Taswira ya moja ya kitongoji cha makazi katika jiji la Mwanza

# Mtambo sasa upo Geita rasmi

Mkuu wa mkoa wa Geita Mhe. Martine Shigela amezindua mtambo mkubwa wa kisasa wa uchimbaji wa visima virefu mkoani Geita.

Uzinduzi huo umefanyika mwezi Juni 2023 katika kijiji cha Ntono kata ya Bukoli wilaya ya Geita ambapo amesema serikali imetumia zaidi ya shilingi bilioni 20 kununua mitambo hiyo ambayo imegawanywa nchini kote na kwa mkoa wa Geita itasaidia kwa kiasi kikubwa kuwezesha uchimbaji wa visima.
Mhe. Shigela ameipongeza RUWASA Mkoa wa Geita kwa utekelezaji wa miradi ya maji vijijini na kutaka mradi wa kisima kirefu katika kijiji cha Ntono kuhakikisha unasambaza maji katika vijiji jirani pamoja na kujenga vituo vya kuchotea maji.

Meneja wa RUWASA Mkoa wa Geita Mhandisi Jabiri Kayilla amesema mtambo huo wa uchimbaji wa visima unahusisha gari ya mitambo ya uchimbaji pamoja na gari la vifaa ukiwa na thamani ya shilingi milioni 600.

Mhandisi Kayilla amesema kwa kuanzia mtambo huo utachimba visima 54 katika wilaya zote tano za mkoa wa Geita ambapo katika wilaya ya Geita kutachimbwa visima 21 kwenye vijiji mbalimbali, Chato Visima 7, Bukombe visima 13, Mbogwe visima 7, Nyang'hwale 6,.

Nao baadhi ya wakazi wa kijiji cha Ntono kata ya Bukoli wilayani humo wameipongeza serikali kwa mradi huo wa kisima cha maji kwa sababu utamaliza kero ya ukosefu wa maji safi na salama katika maeneo yao.



*Mkuu wa Mkoa wa Geita Mhe. Martine Shigela akizindua rasmi mtambo wa uchimbaji visima virefu katika Kijiji cha Ntono, Geita.*



# Siku ya Utumishi wa Umma Barani Afrika

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. George Simbachawene (Mb) amezindua Mkataba wa Huduma ya Mteja, katika kuadhimisha Siku ya Utumishi wa Umma Barani Afrika, katika viwanja vya Nyerere jijini Dodoma.

Mkataba wa Huduma kwa Mteja wa Wizara ya Maji umekabidhiwa kwa Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimaliwatu Bi. Wanyenda Kutta .

Hafla hiyo imehudhuriwa na viongozi mbalimbali kutoka taasisi za umma, ambapo Mkataba huo ni moja ya nyenzo muhimu katika utoajiwa huduma kwa umma na menejimenti ya taasisi za serikali.

Siku ya Utumishi wa Umma Barani Afrika huadhimishwa kila mwaka Juni 23, na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika (AU), lengo likiwa kutambua mchango wa watumishi wa umma katika kuleta maendeleo barani Afrika, pamoja na kutoa tuzo za ubunifu katika kutoa huduma kwa umma.





# TANO za Mwenge mradi wa maji wa Oldonyosambu

Mwenge wa Uhuru umeweka jiwe la msingi katika mradi wa maji wa Oldonyosambu. Mradi huo uliibuliwa mwaka 2020 kutokana na changamoto ya maji yanayotumika kuwa na madini mengi ya floride ambayo madhara yana madhara kwa afya ya binadamu.

Mradi umetekelezwa kwa kutumia fedha za ndani kupitia utaratibu wa wataalamu wa ndani wa Sekta ya Maji (Force Account) na mpaka kukamilika utagharimu shilingi 6,382,532,295.20. Hivi sasa utekelezaji upo asilimia 30 na umeshatumia kiasi cha shilingi 1,311,250,147.3.

Mradi utazalisha maji kiasi cha lita 1,036,800 ambazo zitahudumia wakazi zaidi ya 29,449 wa maeneo ya Oldonyosambu, Lemanda, Oldonyowas na Lesinoni.

Abdala Shaib Kaim, Kiongozi wa mbio za Mwenge Kitaifa 2023 amekagua ujenzi na nyaraka za mradi huo ambapo ameridhika na utekelezaji unaoendelea. Ameridhika viwango na ubora wa ujenzi ikiwa ni pamoja na thamani ya fedha kuakisi matokeo na ubora wa mradi.

Amesema nyaraka ziko vizuri na kupongeza kuwepo kwa cheti cha tathmini ya athari za mazingira na kusisitiza mradi ukamilike kwa wakati kwa kuwa maji ni hitaji la muhimu, pia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha ( AUWSA) kuhakikisha inawasambazia wananchi maji majumbani na kwa ambao hawana uwezo wa kugharamia kupelekewa maji nyumbani wasogezewe huduma karibu katika vituo vya umma vya kuchota maji, kwasababu dhamira ya Serikali inayoongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma ya majisafi na salama.





# Naibu Waziri Mhandisi Mahundi awaagiza DUWASA kufikisha maji Zahanati ya Ntyuka





Naibu Waziri wa Maji Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) amemuagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) Mhandisi Aron Joseph kuhakikisha anafikisha huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza kwenye zahanati ya Ntyuka, kata ya Ntyuka Jijini Dodoma. Agizo hilo amelitoa wakati akizindua mradi wa maji wa Ntyuka-Chimalaa kwa niaba ya Waziri wa Maji. Mradi huo umetekelezwa kwa gharama ya shilingi Milioni 471.8

Amesema dhamira ya serikali ni kuhakikisha inamtua mama ndoo ya maji kichwani huku ikifikisha huduma ya majisafi na salama katika maeneo yote ya huduma za kijamii. Kwa maana hiyo Mkurugenzi ahakikishe Zahanati hiyo iliyoko katika eneo la mradi inafikishiwa huduma ya maji haraka iwekanavyo. Amewahakikishia wananchi wa jiji la Dodoma na Tanzania kwa ujumla kuwa serikali itaendelea na jitihada zake za kuhakikisha huduma za kijamii zinafikiwa na huduma ya majisafi na salama.

Aidha, amewapongeza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa mazingira Dodoma kwa kusimamia vizuri hadi kukamilika kwa mradi huo.

Akitoa taarifa ya mradi huo Mhandisi Aron amesema umetekelezwa kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza imekamilika na inahudumia wakazi wapatao 1,931 katika maeneo ya Ntyuka mtaa wa Chimalaa. Awamu ya pili inatarajiwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2023/24 na itanufaisha wakazi wapatao 2,510 wa mtaa wa Nyerere na hivyo kufanya jumla ya wanufaika wa mradi huo kufikia 4,441.


VIPAUMBELE NA MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2023/24
Kukamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002;
Kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji;
Kuwa na mtandao wa taifa wa maji (National Water Grid);
Kuwa na Mpango Kabambe wa Usambazaji Maji (Water Supply Masterplan);


Utajiri wa Rasilimali za maji Tanzania:
Jumla mita za ujazo bilioni 126 kwa mwaka,
Juu ya ardhi mita za ujazo bilioni 105 na
Chini ya ardhi ni mita za ujazo bilioni 21
Non-perennial
Perennial



Bajeti
WIZARA YA MAJI 2023-2024
Upatikanaji wa Huduma ya Maji Vijijini:
Umeongezeka kutoka 74.5% mwaka 2021 hadi 77% mwaka 2022, na
Idadi ya wananchi wanaopata huduma imeongezeka hadi kufikia 30,209,409.
Mhe. Jumaa Aweso (Mb)
Waziri wa Maji











WIZARA YA MAJI

Bajeti
WIZARA YA MAJI 2023-2024

BAADHI YA MIRADI MIKUBWA YA MAJI INAYOTEKELEZWA MAENEO MBALIMBALI NCHINI

| MRADI | GHARAMA | LENGO | WANUFAIKA |
|---|---|---|---|
| MRADI WA MAJI MUGANGO – KIABAKARI - BUTIAMA | SHILINGI BILIONI 70.5 | KUONGEZA UPATIKANAJI WA MAJI MUGANGO, KIABAKARI NA BUTIAMA | ZAIDI YA WAKAZI 100,000 WA MUGANGO, KIABAKARI NA BUTIAMA NA VIJIJI VILIVYOPO NDANI YA KILOMITA 12 KUTOKA BOMBA KUU. |
| MRADI WA KUBORESHA HUDUMA YA MAJI KATIKA MIJI YA TINDE NA SHELUI | SHILINGI BILIONI 24.75 | KUONGEZA UZALISHAJI WA MAJI KUTOKA LITA MILIONI 68.7 HADI LITA MILIONI 76.3 KWA SIKU. | KUONGEZA UPATIKANAJI WA MAJI TINDE, SHELUI NA VIJIJI JIRANI |
| MRADI WA KUBORESHA HUDUMA YA MAJI KATIKA MIJI 28 | SHILINGI TRILIONI 1.48 | KUBORESHA HUDUMA ZA UPATIKANAJI MAJI KATIKA MIJI YA KALIUWA, SIKONGE, URAMBO, KASULU, MPANDA,KILWA MASOKO, NANYUMBU, IFAKARA, RUJEWA, MAKAMBAKO, NJOMBE, WANGINGOMBE, CHUNYA,CHAMWINO, CHEMBA, SINGIDA, MANYONI, MUGUMU, GEITA, KAYANGA, CHATO, HANDENI, KOROGWE, MUHEZA, PANGANI, MAFINGA, SONGEA, RORYA / TARIME NA MAKONDE. | |
| MRADI WA USAMBAZAJI MAJI KATI YA MAKONGO-DSM NA MJI WA BAGAMOYO, PWANI | SHILINGI BILIONI 71.5 | KUBORESHA MFUMO WA KUHIFADHI NA USAMBAZAJI MAJI | ZAIDI YA WAKAZI 400,000 |





**Kitengo cha Mawasiliano**

Tovuti: www.maji.go.tz